# NITALIHIMIDI JINA LAKO

Zab. 145: 1-2, 8-11, 14, 17 (K)

Wimbo wa Katikati Dominika ya 14 Mwaka "A"

**Con anima**

**Frt. Anga Anselim**
**Ngoheranga (Malinyi)-2023**




1. Ee Mungu wangu Mfalme nitakutukuza,
   Nitalihimidi jina lako milele **na mile-le**/
   Kila siku nitakuhimidi,
   Nitalisifu jina lako milele **na mile-le**.

2. Bwana ana fadhili, ni mwingi wa huruma,
   Si mwepesi wa hasira, ni mwingi **wa rehe-ma**.
   Bwana ni mwema kwa watu wote,
   Na rehema zake zi juu ya kazi **zake zo-te.**

3. Ee Bwana, kazi zako zote zitakushukuru,
   Na wacha Mungu wako wata**kuhimi-di.**
   Wataunena utukufu wa ufalme wako,
   Na kuuhadithia u**weza wa-ko.**

4. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,
   Na mwenye fadhili juu ya kazi **zake zo-te.**
   Bwana huwategemeza wote waangukao,
   Huwainua wote walioina**mia chi-ni.**

@+255 789 774 414